NITAKWENDA WAPI KWA MTIHANI WANGU WA KUCHUNGUZA MATIBABU YA WAKIMBIZI?

Msimamizi wa kesi yako atakusaidia kupanga miadi ya Mtihani wako wa **Uchunguzi wa Matibabu ya Wakimbizi.** Watakuambia ni kliniki gani utakayoenda.

Hii hapa orodha **ya kliniki za afya za Uchunguzi wa Matibabu ya Wakimbizi** zilizo na kandarasi:

ZALINI ZA HUDUMA YA AFYA

IDARA YA AFYA WILAYA YA KATI
1137 SOUTH LOCUST STREET
GRAND ISLAND, NE 68801
308-385-5175

CHI HEALTH CLINIC – UNIVERSITY CAMPUS
2412 CUMING ST. STE. 200,
OMAHA, NE 68131, 402-717-0380

IDARA YA AFYA KAUNTI YA LINCOLN LANCASTER
3131 O STREET, LINCOLN, NE 68510, 402-441-8065

SIOUXLAND COMMUNITY HEALTH CENTER
1021 NEBRASKA STREET
SIOUX CITY, IA 51105, 402-898-1349

MAWAKALA WA MAKAZI MAPYA

HUDUMA ZA KIJAMII KATOLIKI KUSINI KWA NEBRASKA
2241 O STREET, LINCOLN NE 68510, 402-474-1600

KITUO CHA MAENDELEO YA WAHAMIAJI NA WAKIMBIZI (OMAHA NA LINCOLN)
4223 CENTER STREET OMAHA, NE 68105
121 SOUTH 13th STREET LINCOLN, NE 68508
402-898-1349

BARAZA LA KIMATAIFA LA WAKIMBIZI NA WAHAMIAJI
7315 MAPLE ST., OMAHA NE 68134, 402-949-3470

HUDUMA ZA FAMILIA ZA KILUTHERI MAENEO YA LINCON-GRAND ISLAND-LEXINGTON
2301 O STREET, LINCOLN NE 68510
402-441-7940

HUDUMA ZA FAMILIA ZA KILUTHERI - OMAHA
7929 W CENTER RD OMAHA, NE 68124
402-342-7038

INAGHARIMU PESA NGAPI?

Hakuna gharama ya **Uchunguzi** kwa vikundi vinavyostahiki vya waliofika upya Nebraska.

MIADI NI YA MUDA GANI?

1 - 4 masaa: kwa wazazi na watoto

KUMBUKA

Ili kupata huduma **bora zaidi** kwenye **UCHUNGUZI:**

- **Kamilisha** vipimo vyote
- **Nenda** kwa miadi yote
- **Fika** mapema
- **Peleka karatasi ya uchunguzi wa**
- **mtoto wako shuleni kwao**

NEBRASKA
Good Life. Great Mission.

Mratibu wa Wakimbizi wa Jimbo:
402-480-8394

Mratibu wa Afya ya Wakimbizi wa Jimbo:
402-480-0373

Nebraska

UCHUNGUZI WA MATIBABU YA WAKIMBIZI UCHUNGUZI

Mwongozo

JE, NI NINI UCHUNGUZI WA MATIBABU YA WAKIMBIZI?

HATUA YA 1 Marekani kwa afya yako nzuri

Lazima iwe ndani **ya siku 90 za** tarehe yako ya kuwasili.

Wakimbizi wote wanapaswa kuwa na uchunguzi huu

Miadi 1-3 kwa Kliniki ya Matibabu

Uchunguzi wa mwili wako wote na daktari

Daktari atasoma karatasi zako za matibabu

Vipimo vya maambukizo

Chanjo zinazohitajika kwa Green Card

Omba mkalimani - ni haki yako

NILIMUONA DAKTARI KABLA YA KUJA MAREKANI. KWANINI NITAHITAJI KUONA DAKTARI TENA?

Kabla ya kuja Marekani, uchunguzi wa daktari ulikuwa wa idhini yako ya ombi la **Visa ya Marekani.**

Sasa uko Marekani, unapaswa kuwa na **Mtihani wa Uchunguzi wa Matibabu ya Wakimbizi** ili kuanza na Mtoa Huduma ya Msingi (PCP). **PCP** atakusaidia kuwa na afya njema na kutulia kwa mafanikio Nebraska.

MTOA HUDUMA YA MSINGI (PCP) NI NINI?

Mtoa Huduma wako wa Msingi (PCP) ni daktari katika **Kliniki ya Matibabu** unayoenda ukiwa **mgonjwa,** ukihitaji chanjo au una tatizo na mwili au **akili** yako.

JE, NITAJIANDAAJE KWA AJILI MTIHANI?

- Chukua nyaraka zote za matibabu na utambulisho kwa wanafamilia wote. *Kwa mfano, I94s, pasipoti, karatasi za matibabu, maelezo ya chanjo, kadi za Medicaid.*
- Chukua **orodha** ya dawa, chai, mimea na vitamini ambazo familia yako huchukua.
- Chukua orodha ya mizio, wasiwasi wa kiafya, na maswali yoyote uliyo nayo kwa PCP wako.
- Chukua maji , chakula , nepi , vitabu vya watoto
- Fika **dakika 15** kabla ya wakati wako wa miadi.
- Andika orodha ya Jina Kamili la kila **mwanafamilia**, Tarehe ya Kuzaliwa, na Anwani.
- Unaweza kuchagua daktari wa kiume au daktari wa kike , mwambie msimamizi wa kesi yako.
- Kunywa maji mengi kabla ya kwenda.

SIWEZI KWENDA, NIFANYEJE?

Mpigie simu meneja wa kesi yako.

JE, NITAFANYAJE NIKIFIKA KWENYE KLINIKI YA MATIBABU?

1. Nenda kwenye **dawati** la mbele, waambie wafanyikazi **jina** lako.
2. Keti katika eneo la **kusubiri**. Waulize wafanyakazi ikiwa unahitaji kwenda **msalani.** Usiondoke isipokuwa kwa dharura.
3. Muuguzi **anapoita** jina lako, peleka familia yako kwenye **chumba cha uchunguzi.**
4. PCP atachunguza mwili wako.
5. PCP atauliza maswali kuhusu hisia zako na mwili wako.
6. PCP **atatoa damu yako** kwenye **uchunguzi huu.**

HAKI ZANGU NI ZIPI WAKATI WA UCHUNGUZI?

- Kuomba **nakala** iliyochapishwa ya **Uchunguzi wa Matibabu ya Wakimbizi.**
- Kila mwanafamilia ana haki ya kupata matunzo na huduma za kitaalamu zilizo **sawa**.
- Upatikanaji wa huduma za ukalimani **BURE.**
- Kuwa na daktari wa kiume au wa kike ikiwezekana.
- Kuleta **rafiki.**
- Kwa **faragha:** Faragha yako inalindwa na sheria za Marekani (HIPAA). Taarifa zako zote za kibinafsi na za afya zitasalia kuwa za faragha na za siri.

WATOTO WANGU WANAHITAJI NINI?

Nchini Marekani, kila mtoto anahitaji uchunguzi wa daktari na chanjo **kabla** ya kwenda shule.

PCP atakupa **karatasi** ya uchunguzi uliokamilika wa mtoto wako. Ipeane karatasi hii **shuleni.**